

---

# MAKUBALIANO YA 2005 YA ULINZI NA UKUZAJI WA VIELELEZO VYA TAMADUNI ANUWAI

---



United Nations  
Educational, Scientific and  
Cultural Organization



Vielelezo vya Tamaduni  
Anuwai



# MAKUBALIANO YA ULINZI NA UKUZAJI WA VIELELEZO VYA TAMADUNI ANUWAI

---

---

---

Paris, 20 Oktoba 2005

Kongamano Kuu la Umoja wa Mataifa linalohusisha mambo ya Kielimu, Kisayansi na Kitamaduni lililofanyika Paris mnamo tarehe 3 – 21 Oktoba 2005 kwenye kikao chake cha 33,

---

**Kwa kuthibitisha** kwamba tamaduni anuwai ndiyo tabia inayomtambulisha binadamu,

---

**Kwa kutambua** kwamba tamaduni anuwai huunda urithi wa pamoja wa binadamu, kwa hivyo unahitaji kutunzwa na kuhifadhiwa kwa manufaa ya wote,

---

**Kwa kufahamu** kwamba tamaduni anuwai huumba dunia tajiri yenye mseto wa mambo yanayopanua nafasi ya kuchagua, huku zikikuza uwezo na maadili ya binadamu, na kwa hivyo ni chemchemi muhimu ya maendeleo endelevu ya jamii mbalimbali, watu na mataifa,

---

**Kwa kukumbuka** kwamba tamaduni anuwai zinazostawi ndani ya utaratibu wa kidemokrasia, uvumilivu, haki za kijamii na

heshima miongoni mwa watu na tamaduni hizo zao ni lazima ili kujenga amani na usalama katika viwango vya mashinani, kitaifa na kimataifa,

---

**Kwa kusherehekea** umuhimu wa tamaduni anuwai katika kutambua kikamilifu uhuru na haki za binadamu zilizotangazwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu pamoja na vyombo vingine vinavyotambuliwa ulimwenguni,

---

**Kwa kusisitiza** umuhimu wa kujumuisha utamaduni kama kipengele muhimu katika sera za maendeleo ya kitaifa na kimataifa, na katika ushirikiano wa maendeleo ya kimataifa, kwa kuzingatia pia Azimio la Milenia la Umoja wa Mataifa (2000) pamoja na msisitizo wake wa kutokomeza umaskini,

---

**Kwa kuzingatia** kwamba utamaduni huchukua maumbo anuwai kutegemea wakati na mahali, na kwamba uanuwai huu hujumuisha upekee na wingi wa tofauti za watu pamoja na jamii zenye vielelezo vya kitamaduni ambavyo hujenga pamoja ubinadamu,

---

**Kwa kutambua** umuhimu wa ujuzi wa kiasili kama chanzo cha utajiri usiogusika na ule unaogusika, hasa mifumo ya ujuzi wa kiasili wa wenyeji na mchango wao katika maendeleo endelevu, pamoja na umuhimu wa kuulinda na kuukuza,

---

**Kwa kutambua** haja ya kuchukua hatua za kulinda vielelezo anuwai vya kitamaduni pamoja na yale yaliyomo hasa pale ambapo vielelezo hivyo vinakumbwa na tisho la kupotea kabisa au kuharibiwa,

---

**Kwa kusisitiza** umuhimu wa utamaduni kama njia ya kujenga

mshikamano kwa ujumla, na hasa ule uwezo wake wa kuendeleza nafasi na majukumu ya wanawake katika jamii,

---

**Kwa kufahamu** kwamba tamaduni anuwai hupata nguvu kutokana na uhuru wa kuchangiana mawazo, na kwamba hurutubishwa na kule kupokezana mawazo na maingiliano baina ya tamaduni mbalimbali,

---

**Kwa kukubali** kwamba uhuru wa kuchangia mawazo, uhuru wa kujieleza na uhuru wa habari, kukiwemo pia vyombo anuwai vya mawasiliano, huwezesha vielelezo vya tamaduni mbalimbali kujiimarisha miongoni mwa jamii mbalimbali,

---

**Kwa kutambua** kwamba vielelezo vya tamaduni anuwai, vikiwemo vielelezo vya tamaduni asilia ni jambo muhimu linalowaruhusu watu binafsi na watu mbalimbali kuzungumza na kuchangiana mawazo na maadili kwa wengine,

---

**Kwa kukumbuka** kwamba lugha anuwai ni kipengele muhimu cha tamaduni anuwai, na kuthibitisha jukumu muhimu ambalo elimu hutekeleza katika kulinda na kukuza vielelezo vya kitamaduni,

---

**Kwa kuzingatia** umuhimu wa nguvu za tamaduni mbalimbali, kukiwemo zile tamaduni za jamii ndogo ndogo na zile za watu asilia kama zinavyojitambulisha kupitia kwa uhuru wao wa kubuni, kusambaza na kuenenza vielelezo vya tamaduni zao asilia, na kupata nafasi ya kuvitumia pia ili kuzinufaisha jamii hizo kimaendeleo,

---

**Kwa kusisitiza** jukumu kuu la utangamano wa kitamaduni na ubunifu ambao hurutubisha na kuleta upya tena katika vielelezo

vya kitamaduni, na kwa hivyo kuboresha kazi inayotekelezwa na wale wanaohusika na maendeleo ya utamaduni ili kuleta maendeleo ya jamii kwa ujumla,

---

**Kwa kutambua** umuhimu wa haki miliki kwa lengo la kuwahimili wale wanaohusika katika ubunifu wa kitamaduni,

---

**Kwa kuridhishwa** kwamba shughuli za kitamaduni, bidhaa na huduma zote zina umuhimu wa kiuchumi na uasili wa kitamaduni kwa sababu zinapitisha utambulisho, maadili na maana, na kwa hivyo zisichukuliwe tu kama vitu vyenye thamani ya kibiashara,

---

**Kwa kuona** kwamba ijapokuwa mifanyiko ya utandawazi inayowezeshwa na maendeleo ya haraka ya habari na teknolojia ya mawasiliano, na kwamba mifanyiko hiyo imeweza kuleta utangamano wa hali ya juu miongoni mwa tamaduni mbalimbali, imeleta changamoto pia katika uanuwai wa kitamaduni kama vile hatari ya kutolingana baina ya nchi tajiri na zile maskini,

---

**Kwa kufahamu** jukumu mahususi la UNESCO katika kuhakikisha kwamba tamaduni anuwai zinaheshimiwa, mbali na kupendekeza maafikiano ya kimataifa itakapohitajika, ili kukuza mtiririko wa mawazo kupitia kwa maneno au vinginevyo,

---

**Kwa kurejelea** vifungu kutoka katika vyombo vya kimataifa vilivyokubaliwa na UNESCO na vinavyohusiana na tamaduni anuwai, na utekelezwaji wa haki za kitamaduni, hasa lile Azimio la Kimataifa kuhusu Tamaduni Anuwai la mwaka wa 2001,

---

**Linakubali** Makubaliano haya tarehe 20 Oktoba 2005.



# MALENGO NA KANUNI ELEKEZI

---

# KIFUNGU 1

## MALENGO

---

---

---

Malengo ya Makubaliano haya ni:

- a) Kulinda na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai;
- b) Kuimarisha hali ambapo tamaduni zitastawi na kutangamana bila vikwazo kwa manufaa ya kila mojawapo;
- c) Kuhimiza kuwepo kwa usemezano miongoni mwa tamaduni mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba kuna mabadilishano ya kitamaduni duniani ili kuleta utangamano wa kitamaduni wenye heshima na amani;
- d) Kuendeleza utangamano wa kitamaduni ili kujenga mwingiliano wa kitamaduni kwa manufaa ya kuimarisha uhusiano mwema miongoni mwa watu;
- e) Kukuza heshima katika vielelezo vya tamaduni anuwai na kuimarisha ule utambuzi wa maadili yavyo katika viwango vya mashinani, kitaifa na kimataifa;
- f) Kudhihirisha kwa msisitizo umuhimu wa uhusiano baina ya utamaduni na maendeleo ya nchi zote hasa zile zinazoendelea, na kuunga mkono juhudi zinazofanywa kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha kwamba uhusiano huu umetambuliwa;
- g) Kutambua upekee wa shughuli za kitamaduni, bidhaa zake pamoja na huduma kama vyombo vya utambulisho,



maadili na maana husika;

- h) Kudhihirisha kwa msisitizo haki kuu za madola za kudumisha, kutumia na kutekeleza sera na hatua muafaka za kulinda na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai katika maeneo yao;
- i) Kuimarisha uhusiano wa kimataifa na umoja wa ushirikiano ili kuzidisha uwezo wa nchi zinazoendelea katika kulinda na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai.

## KIFUNGU 2

### KANUNI ELEKEZI

---

---

---

---

- ① **Kanuni ya kuheshimu haki za binadamu na uhuru wa kimsingi**

Tamaduni anuwai zinaweza kulindwa na kukuzwa iwapo haki za binadamu na uhuru wa kimsingi kama vile uhuru wa kujieleza, uhuru wa habari na mawasiliano pamoja na uwezo wa watu binafsi kuchagua vielelezo vya kitamaduni vitahakikishwa. Hakuna mtu atakayetumia vifungu vya Makubaliano haya ili kukandamiza haki za binadamu na uhuru wa kimsingi kama inavyoelezwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu au kuhakikishiwa na sheria ya kimataifa, au hata kupunguza upeo wa uhuru wa haki hizo.
- ② **Kanuni ya mamlaka**

Kulingana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa na kanuni ya sheria ya kimataifa, madola yana haki na mamlaka ya kuteua na kutumia hatua na sera zao kwa ajili ya kulinda na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai katika maeneo yao.

- ③ **Kanuni ya usawa wa hadhi na heshima kwa tamaduni zote**  
Ulinzi na ukuzaji wa vielelezo vya tamaduni anuwai unamaanisha kuwa na hadhi sawa pamoja na kuheshimu tamaduni zote, zikiwemo zile tamaduni za watu wanaotoka katika jamii ndogo ndogo na zile za kienyeji.
- ④ **Kanuni ya umoja na ushirikiano wa kimataifa**  
Umoja na ushirikiano wa kimataifa hauna budi kulenga katika kuziwezesha nchi hasa zile zinazoendelea kubuni na kuimarisha njia zao za vielelezo vya kitamaduni, kukiwemo viwanda vya kitamaduni vinavyoanza au vilivyoimarika tayari katika viwango vya mashinani, kitaifa na kimataifa.
- ⑤ **Kanuni ya kukamilishana katika maendeleo ya kiuchumi na kitamaduni**  
Kwa vile utamaduni ni mojawapo ya chemchemi za maendeleo, vipengele vya maendeleo ya kitamaduni ni muhimu pia kama vilivyo vile vya kiuchumi ambavyo watu binafsi na watu wote kwa jumla wana haki ya kimsingi ya kushiriki na kufurahia.
- ⑥ **Kanuni ya Maendeleo endelevu**  
Tamaduni anuwai ni rasilmali tajiri ya watu binafsi na jamii kwa jumla. Kule kulinda, kukuza na kudumisha tamaduni anuwai ni hitaji muhimu la maendeleo endelevu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.
- ⑦ **Kanuni ya Usawa wa upatikanaji**  
Usawa wa upatikanaji wa vielelezo anuwai vya tamaduni mbalimbali duniani kote na upatikanaji wa tamaduni kwa njia ya vielelezo na usambazaji huhusisha mambo muhimu yatakayozidisha uanuwai wa kitamaduni na uelewa wa pamoja.

## 8 Kanuni ya Uwazi na usawa

Madola yatakapoweka hatua za kuunga mkono vielelezo vya tamaduni anuwai, yatahitaji pia kutafuta mbinu za kukuza vielelezo hivyo kwa njia inayofaa na iliyo wazi kwa tamaduni zingine duniani, mbali na kuhakikisha kwamba hatua hizo zinalingana na malengo yanayozingatiwa katika Makubaliano haya.



# UPEO NA UTEKELEZAJI

---

## KIFUNGU 3

# UPEO NA UTEKELEZAJI

---

---

---

Makubaliano haya yatahusisha sera na hatua zilizokubaliwa na Nchi Husika kuhusiana na ulinzi na ukuzaji wa vielelezo vya tamaduni anuwai



# UFAFANUZI WA MAANA

---

# KIFUNGU 4

## UFANUZI WA MAANA

---

---

---

Kwa mujibu wa Makubaliano haya, inamaanisha kwamba:

- 1 Tamaduni anuwai**

“Tamaduni anuwai” ni jinsi ambavyo tamaduni za makundi na jamii mbalimbali hujieleza. Vielelezo hivi hupitishwa ndani na pia miongoni mwa makundi na jamii mbalimbali. Tamaduni anuwai hujidhihirisha sio tu kupitia kwa jinsi turathi za kitamaduni zinavyojibainisha, kukuzwa na kusambazwa kupitia kwa njia mbalimbali za vielelezo vya kitamaduni, lakini pia kupitia kwa njia mbalimbali za ubunifu wa kisanaa, uzalishaji wa vitu, uenezaji, usambazaji na uburudishaji kwa kutumia teknolojia na njia zozote zile.
- 2 Yanayohusishwa katika utamaduni**

“Yanayohusishwa katika utamaduni” hapa yanarejelea maana za kiishara, upana wa kisanaa na maadili ya kitamaduni ambayo yanatokana na au yanabainisha utambulisho fulani wa kitamaduni.
- 3 Vielelezo vya kitamaduni**

“Vielelezo vya kitamaduni” ni vile vielelezo vinavyotokana na ubunifu wa watu binafsi, wa makundi au wa jamii mbalimbali na ambao huhusisha mambo ya kitamaduni.
- 4 Shughuli za kitamaduni, bidhaa na huduma.**

“Shughuli za kitamaduni, bidhaa na huduma” ni zile shughuli, bidhaa na huduma ambazo huchukuliwa kama sifa mahususi,

matumizi au makusudio fulani ambayo hujumuisha au kupitishia vielelezo vya kitamaduni bila kujali thamani ya kibiashara inayofungamanishwa na vitu hivyo. Shughuli za kitamaduni huweza kukamilika jinsi zilivyo au pia zinaweza kuchangia katika uzalishaji wa bidhaa au huduma.

#### 5 **Viwanda vya Kitamaduni**

“Viwanda vya kitamaduni” ni vile viwanda vinavyozalisha na kusambaza bidhaa za kitamaduni au huduma kama inavyofafanuliwa katika ibara ya 4 hapo juu.

#### 6 **Sera na hatua za kitamaduni**

“Sera na hatua za kitamaduni” ni zile zinazohusiana na utamaduni, hata kama ziko katika kiwango cha mashinani, kitaifa, kieneo au kimataifa na ambazo zinazingatia au zimeundwa ili kuwa na athari ya moja kwa moja kwa vielelezo vya kitamaduni vya watu binafsi, makundi au jamii mbalimbali. Sera na hatua hizo pia zinahusiana na ubunifu, uzalishaji, uenezaji, usambazaji wa vielelezo pamoja na upatikanaji wa nafasi za kufanyia shughuli za kitamaduni, za bidhaa na huduma.

#### 7 **Ulinzi**

“Ulinzi” ni kule kuchukuliwa kwa hatua zinazolenga kuhifadhi, kulinda na kupanua vielelezo vya tamaduni anuwai. “Kulinda” kunamaanisha kuchulikwa kwa hatua kama hizo.

#### 8 **Mwingiliano wa kitamaduni**

“Mwingiliano wa kitamaduni” ni kule kuwepo na mwingiliano sawa wa tamaduni anuwai na ule uwezekano wa kuzalisha kwa pamoja vielelezo vya kitamaduni kupitia kwa usemezano na kuheshimiana.





# HAKI NA WAJIBU WA NCHI HUSIKA

---

## KIFUNGU 5

# SHERIA YA JUMLA KUHUSU HAKI NA WAJIBU

---

---

---

- 1 Kwa kukubaliana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Kanuni za Sheria ya kimataifa na vyombo vya haki za binadamu vinavyotambuliwa duniani, Nchi Husika katika makubaliano haya zinakubali kwa dhati haki ya mamlaka yao kubuni na kutekeleza sera zao za kitamaduni, kuteua hatua za kulinda na kukuza tamaduni anuwai pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa.
- 2 Nchi inapotekeleza sera na kuchukua hatua za kulinda na kukuza tamaduni anuwai katika maeneo yake, basi sera na hatua hizo zitalingana na masharti ya Makubaliano haya.

## KIFUNGU 6

# HAKI ZA NCHI KATIKA KIWANGO CHA KITAIFA

---

---

---

- 1 Kila Nchi itachukua hatua zinazolenga kulinda na kukuza tamaduni anuwai katika eneo lake kulingana na utaratibu wa sera zake za kitamaduni na hatua itakazochukua kama inavyoelezwa katika Kifungu cha 4.6 huku ikizingatia hali na mahitaji yake;

- 2) Hatua kama hizo zitashirikisha yafuatayo:
- a) Hatua zenye kufuata utaratibu mahususi zitakazolenga kulinda na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai;
  - b) Hatua zinazofaa ili kuimarisha nafasi ambayo itaruhusu utekelezaji wa shughuli za kitamaduni nchini, bidhaa na huduma pamoja na yale yote ya kitamaduni yanayopatikana nchini kuhusiana na kubuni, kuzalisha, kueneza na kufurahia shughuli hizo za kitamaduni nchini, hatua za utekelezaji wa bidhaa na huduma kukiwemo pia uwezeshwaji wa kutumia lugha katika kutekeleza shughuli, bidhaa na huduma za kitamaduni;
  - c) Hatua zinazolenga kuimarisha viwanda na shughuli nyingine huru za kitamaduni nchini hasa katika sekta zisizo rasmi, upatikanaji wa njia za uzalishaji mali, uenezaji na usambazaji wa shughuli za kitamaduni, bidhaa na huduma;
  - d) Hatua zitakazolenga usaidizi wa kifedha kwa umma;
  - e) Hatua zitakazolenga kuyahamasisha mashirika yasiyo ya kibiashara, zikiwemo pia taasisi za umma na zile za kibinafsi, wasanii na wataalamu wengine wa kitamaduni, ili kuanzisha na kukuza ubadilishanaji na uenezaji wa mawazo, vielelezo na shughuli za kitamaduni, bidhaa na huduma, na kadhalika kutia watu moyo wa ujasiriamali na ubunifu katika shughuli zao;
  - f) Hatua zitakazolenga kujenga na kusaidia taasisi za umma kama inavyofaa.
  - g) Hatua zitakazohakikisha kuwalea na kuwasaidia wasanii na wale wanaohusika na ubunifu wa vielelezo vya kitamaduni;

- h) Hatua zitakazolenga ukuzaji wa vyombo anuwai vya habari, na pia kupitia kwa huduma ya utangazaji kwa umma.

## KIFUNGU 7

# HATUA ZA KUKUZA VIELELEZO VYA KITAMADUNI

---

---

---

- ① Nchi zitajitahidi kuimarisha hali muafaka katika maeneo yao itakayowahimiza watu binafsi na makundi ya kijamii:
  - a) Kubuni, kuzalisha, kueneza, kusambaza, pamoja na wao kuwezesha kuvipata vielelezo vyao vya kitamaduni wenyewe huku Nchi hizo zikizingatia hali maalumu za mahitaji ya wanawake na makundi mengine ya kijamii, kukiwemo pia watu kutoka katika jamii ndogo ndogo na za kiasili;
  - b) Kuwezesha kupata vielelezo vya tamaduni anuwai ndani ya maeneo yao pamoja na vile vilivyo katika nchi zingine ulimwenguni.
- ② Nchi zitajitahidi kutambua mchango mkubwa wa wasanii na wale wanaohusika na mfanyiko mzima wa ubunifu, pamoja na kutambua jamii za kitamaduni zilizo mashinani na mashirika yanayounga mkono kazi za kitamaduni pamoja na jukumu lao la kutunza vielelezo vya tamaduni anuwai.

## KIFUNGU 8

# HATUA ZA KULINDA VIELELEZO VYA KITAMADUNI

---

---

---

- 1 Nchi inaweza kuamua kwamba kuna hali iliyopo ambapo vielelezo vya kitamaduni katika eneo lake vinakabiliwa na hatari ya kuangamia, kutishiwa uwepo wake au hata kuhitaji uhifadhi wa haraka, na kwa hivyo kuchua hatua ya kuvihifadhi ambayo haitaleti athari yoyote katika masharti yaliyo katika Vifungu vya 5 na 6.
- 2 Nchi zinaweza kuchukua hatua zote zinazofaa ili kulinda na kuhifadhi vielelezo vya kitamaduni kulingana na vile ilivyoelezwa kwenye ibara ya 1, kwa njia ambayo inaafiki masharti ya Makubaliano haya.
- 3 Nchi itatoa ripoti kwa Kamati ya Serikali za Nchi inayorejelewa pia katika Kifungu cha 23 kuhusu hatua zote ambazo imechukua ili kukabiliana na hali hizo za dharura, pamoja na kutoa mapendekezo yanayofaa.

## KIFUNGU 9

### KUPOKEZANA HABARI NA UWAZI

---

---

---

Nchi zitawajibika:

- a) Kutoa katika ripoti zao habari zinazofaa kwa UNESCO kila baada ya miaka minne kuhusu hatua zilizochukua kulinda na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai katika maeneo yao na katika viwango vya kimataifa pia.
- b) Kuteua pahali maalumu pa kupokezana habari kwa mujibu wa Makubaliano haya.
- c) Kupokezana na kubadilishana habari zinazohusiana na ulinzi na ukuzaji wa vielelezo vya tamaduni anuwai.

## KIFUNGU 10

### ELIMU NA UTAMBUZI WA UMMA

---

---

---

Nchi zitawajibika:

- a) Kuhimiza watu kuelewa na kukuza umuhimu wa kulinda vielelezo vya tamaduni anuwai hasa kupitia kwa programu za kielimu na kujenga utambuzi mpana kwa umma.
- b) Kushirikiana na nchi zingine pamoja na mashirika ya kimataifa na kimaeneo katika kufaulisha lengo la Kifungu hiki.

- c) Kuendelea kuhimiza ubunifu pamoja na kuimarisha uwezo wa uzalishaji kupitia kuanzishwa kwa programu za kielimu, utoaji wa mafunzo na uzalishaji katika viwanda vya kitamaduni. Hatua hizi hazina budi kutekelezwa kwa njia ambayo haitaleta athari mbaya kwa ule uzalishaji wa kiasili.

## KIFUNGU 11

### KUSHIRIKI KWA RAIA

---

---

---

Nchi zinatambua jukumu muhimu la raia katika kulinda na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai. Kwa hivyo zitahimiza kushiriki kikamilifu kwa raia katika jitihada zao za kufanikisha malengo ya Makubaliano haya.

## KIFUNGU 12

### UKUZAJI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

---

---

---

Nchi zitajitahidi kuimarisha ushirikiano baina ya nchi moja na nyingine, ushirikiano wa kimaeneo na kimataifa ili kuweka hali inayofaa ya kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai, hasa kwa kuzingatia hali zinazorejelewa katika Vifungu vya 8 na 17 ili:

- a) Kurahisisha usemezano miongoni mwa Nchi mbalimbali kuhusu sera ya kitamaduni;
- b) Kuimarisha uwezo wa umma wa kusimamia na kuweka mikakati katika taasisi za kitamaduni kupitia kwa ubadilishanaji wa kitamaduni katika viwango vya kitaaluma na kimataifa, pamoja na kupokezana desturi ambazo ni bora zaidi;
- c) Kuimarisha ubia wa raia na miongoni mwa raia, pamoja na mashirika yasiyokuwa ya serikali na sekta za kibinafsi katika kuendeleza na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai;
- d) Kukuza matumizi ya teknolojia mpya na kuhimiza ubia wa raia ili kuimarisha upokezanaji wa habari na uelewa wa kitamaduni kwa lengo la kuendeleza vielelezo vya tamaduni anuwai;
- e) Kuhimiza kukamilishwa kwa mapatano yanayohusu uzalishaji na usambazaji wa pamoja.

## KIFUNGU 13

# KUHUSISHA UTAMADUNI KATIKA MAENDELEO ENDELEU

---

---

---

Nchi zitajitahidi kuhusisha utamaduni katika sera zao za maendeleo katika viwango vyote ili kuimarisha mazingira yanayofaa kwa maendeleo endelevu, na katika utaratibu huu ziweze kuendeleza vipengele vinavyohusu ulinzi na ukuzaji wa vielelezo vya tamaduni anuwai.



# KIFUNGU 14

## USHIRIKIANO ILI KULETA MAENDELEO

---

---

---

Nchi zitajitahidi kuunga mkono ushirikiano ili kuleta maendeleo endelevu na kupunguza umaskini, hasa kuhusiana na mahitaji maalumu ya nchi zinazoendelea kwa lengo la kukuza uibukaji wa sekta ya kitamaduni kupitia kwa njia zifuatazo:

- a) Kustawisha viwanda vya kitamaduni katika nchi zinazoendelea kupitia kwa:
  - i) Kubuni na kustawisha mazao ya kitamaduni na kuimarisha uwezo wa kuyasambaza katika nchi zinazoendelea;
  - ii) Kusaidia kupata nafasi zaidi katika soko la ulimwengu na katika nyenzo za usambazaji wa kimataifa wa shughuli zao za kitamaduni, bidhaa na huduma zao;
  - iii) Kuwezesha uanzishwaji wa masoko mashinani na katika maeneo;
  - iv) Kuimarisha hatua muafaka ikiwezekana, zitakazowezesha shughuli, bidhaa na huduma za kitamaduni kutoka nchi zinazoendelea kuingizwa katika nchi zilizostawi;
  - v) Kuwasaidia na kuwawezesha wasanii wa nchi zinazoendelea katika kazi zao za kiubunifu na urahisi wa kuzuru sehemu mbalimbali;

- vi) Kuhimiza ushirikiano unaofaa baina ya nchi zilizostawi na zile zinazoendelea katika maeneo kama vile muziki na filamu.
- b) Kujenga uwezo kupitia kwa ubadilishanaji wa habari, tajriba na ujuzi pamoja na kufunza watu uwezo wa kuweka mikakati na usimamizi, uimarishaji wa sera na utekelezaji, ukuzaji na usambazaji wa vielelezo vya kitamaduni, uendelezaji wa shughuli za kibiashara katika viwango vya udogo, wastani au hata udogo sana, matumizi ya teknolojia pamoja na ujenzi na uhamishaji wa maarifa katika nchi zinazoendelea, hasa katika sekta za umma na za kibinafsi;
- c) Uhamishaji wa teknolojia kupitia kuanzishwa kwa vichocheo vifaavyo ili kuhamasisha teknolojia na ujuzi hasa katika sehemu za viwanda vya kitamaduni na katika shughuli za kibiashara;
- d) Usaidizi wa kifedha kupitia:
  - i) Kuanzishwa kwa Hazina ya Kimataifa ya Tamaduni Anuwai kama inavyoelezwa katika Kifungu cha 18;
  - ii) Kupatikana kwa usaidizi rasmi wa kimaendeleo kukiwemo usaidizi wa kiteknolojia ili kuhamasisha na kuunga mkono ubunifu;
  - iii) Kuwa na njia nyingine za usaidizi wa kifedha kama vile mikopo yenye viwango vya chini vya riba, ufadhili wa kifedha pamoja na njia nyingine za ufadhili.

## KIFUNGU 15

# MIPANGILIO YA USHIRIKIANO

---

---

---

Nchi zitahimiza kuanzishwa kwa ubia miongoni na ndani ya sekta za umma na za kibinafsi pamoja na mashirikia yasiyokuwa ya kibiashara ili kushirikiana na nchi zinazoendelea katika kuboresha uwezo wao wa kulinda na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai. Ubia huu wa kipekee utasisitiza pia maendeleo zaidi ya miundo msingi, rasilmali ya binadamu na sera, ukiwemo pia ubadilishanaji wa shughuli za kitamaduni, bidhaa na huduma kulingana na mahitaji halisi ya nchi zinazoendelea.

## KIFUNGU 16

# UPENDELEO KWA NCHI ZINAZOENDELEA

---

---

---

Nchi zilizostawi zitasaidia katika ubadilishanaji wa kitamaduni na nchi zinazoendelea kwa kuzipa nchi hizi upendeleo kwa wasanii wao, wataalamu na wajuzi wengine wa kitamaduni, bidhaa na huduma zao za kitamaduni kupitia kwa taratibu zifaazo za kitaasisi na kisheria.

## KIFUNGU 17

# USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KATIKA HALI ZA TISHIO KUBWA KWA VIELELEZO VYA KITAMADUNI

---

---

---

Nchi zitashirikiana katika kutoa usaidizi miongoni mwao na hasa kwa nchi zinazoendelea hasa kuhusu hali zinazorejelewa kwenye Kifungu cha 8.

## KIFUNGU 18

# HAZINA YA KIMATAIFA KWA TAMADUNI ANUWAI

---

---

---

- ① Hazina ya kimataifa kwa tamaduni anuwai ambayo hapa inajulikana kama “Hazina” imeanzishwa.
- ② Hazina hii itahusisha hazina za dhamana ambazo zitakuwa zimeanzishwa kulingana na Kanuni za Kifedha za UNESCO.
- ③ Rasilmali za Hazina zitahusisha:
  - a) Michango ya hiari inayotolewa na Nchi Husika;
  - b) Fedha zilizotengwa kwa lengo hili na Kongamano Kuu la UNESCO;
  - c) Michango, zawadi au mapokeo kutoka kwa madola

mengine, mashirika na kutoka kwa programu za Umoja wa Mataifa, mashirika mengine ya kimaeneo au kimataifa, mashirika ya umma, yale ya kibinafsi au watu binafsi;

- d) Riba zozote zinazotokana na rasilmali za Hazina hii;
- e) Fedha zinazokusanywa kutokana na shughuli zinazofanywa kwa manufaa ya Hazina hiyo;
- f) Rasilmali nyinginezo zinazoruhusiwa na sheria za Hazina hii.

- 4 Matumizi ya rasilmali ya Hazina yataamuliwa na Kamati ya Serikali za Nchi Husika kwa kuzingatia mwongozo ulioamuliwa na Kongamano la Nchi Husika linalorejelewa katika Kifungu cha 22.
- 5 Kamati ya Serikali za Nchi inaweza kukubali michango na namna nyingine za usaidizi kwa makusudio ya jumla au maalumu kuhusiana na miradi mahususi, iwapo miradi hiyo imeidhinishwa na Kamati hiyo.
- 6 Hakuna masharti ya kisiasa, kiuchumi au mengine yoyote yasiyolingana na malengo ya Makubaliano haya yatahusishwa na michango itakayotolewa kwa Hazina hii.
- 7 Nchi zitajitahidi kutoa michango kwa hiari kupitia kwa utaratibu maalumu ili kutekeleza Makubaliano haya.

## KIFUNGU 19

# UBADILISHANAJI, UCHANGANUZI NA USAMBAZAJI WA HABARI

---

---

---

- ① Nchi zinakubali kubadilishana habari na kupokezana ujuzi juu ya ukusanyaji wa data na takwimu kuhusu vielelezo vya tamaduni anuwai pamoja na desturi nzuri za kulinda na kukuza uanuwai huu.
- ② Kupitia kwa matumizi ya taratibu zilizoko katika ofisi yake, UNESCO itasaidia katika ukusanyaji, uchanganuzi na usambazaji wa habari zote muhimu, zikiwemo takwimu na desturi nzuri za kuzingatiwa.
- ③ UNESCO pia itaanzisha na kujaliza upya kanzi data ya sekta mbalimbali, mashirika ya kiserikali, kibinafsi na yale yasiyokuwa ya kibiashara ambayo yanajihusisha na vielelezo vya kitamaduni.
- ④ Ili kuwezesha ukusanyaji wa data, UNESCO itajihusisha na utoaji wa mafunzo kuwezesha watu kuwa na ujuzi hasa kutoka katika nchi zinazotoa maombi ya kutaka usaidizi huo.
- ⑤ Ukusanyaji wa habari zinazotambuliwa katika Kifungu hiki zitajaliza habari zilizokusanywa chini ya Kifungu cha 9.



# UHUSIANO NA VYOMBO VINGINE

---

## KIFUNGU 20

# UHSIANO NA MIKATABA MINGINE: KUSAIDIANA, KUKAMILISHANA NA KUTODUNISHA

---

---

---

- ① Nchi zinatambua kwamba zitatekeleza majukumu yao kwa imani chini ya Makubaliano haya na mikataba yote mingine zilizoidhinisha. Hivyo basi, bila kudunisha Makubaliano haya kupitia kwa mkataba wowote ule,
  - a) Nchi zitakuza kule kusaidiana baina ya Makubaliano haya na mikataba mingine ambayo ziliidhinisha; na
  - a) Pale zinapofasiri na kutumia mikataba mingine zilizoidhinisha au pale Nchi hizo zinapoingia kuidhinisha majukumu mengine ya kimataifa, basi zitazingatia masharti husika yaliyomo katika Makubaliano haya.
- ② Katika Makubaliano haya, hakuna chochote ambacho kitafasiriwa ili kuonekana kama kinachobadilisha haki na majukumu ya Nchi Husika chini ya mikataba mingine yoyote ambayo ziliidhinisha.



## KIFUNGU 21

# USHAURI NA URATIBU WA KIMATAIFA

---

---

---

Nchi Husika zinajitolea kuendeleza malengo na kanuni za Makubaliano haya katika mikutano mingine ya kimataifa. Kutokana na hili basi, Nchi hizo Husika zitashauriana miongoni mwao kama inavyotakikana huku zikizingatia malengo na kanuni za Makubaliano haya.



# MATAWI YA MAKUBALIANO

---

## KIFUNGU 22

# KONGAMANO LA NCHI HUSIKA

---

---

---

- ① Kongamano la Nchi Husika litaanzishwa. Kongamano la Nchi Husika litakuwa jumuiiko kuu la Makubaliano haya.
- ② Kongamano la Nchi Husika litakutana katika kikao cha kawaida ikiwezekana baada ya kila miaka miwili huku likiungana na Kongamano Kuu la UNESCO. Kongamano la Nchi Husika likiamua pia, linaweza kukutana katika kikao kisichokuwa cha kawaida, au pale Kamati ya Serikali za Nchi inapokea ombi la kufanya hivyo iwapo kutakuwa na akidi ya thuluthi moja ya Nchi Husika.
- ③ Kongamano la Nchi Husika litateua sheria zake za utendakazi.
- ④ Shughuli za Kongamano la Nchi Husika ni pamoja na:
  - a) Kuchagua wanachama wa Kamati ya Serikali za Nchi;
  - b) Kupokea na kuchunguza ripoti kutoka kwa Nchi wanachama wa Makubaliano haya zinazowasilishwa kupitia kwa Kamati ya Serikali za Nchi;
  - c) Kuidhinisha mipangilio ya kazi iliyotayarishwa na Kamati ya Serikali za Nchi kulingana na matakwa ya Kongamano hilo la Nchi Husika;
  - d) Kuchukua hatua zozote zingine ambazo Kongamano la Nchi Husika linafikiria ni muhimu ili kuendeleza malengo ya Makubaliano haya.

## KIFUNGU 23

# KAMATI YA SERIKALI ZA NCHI HUSIKA

---

---

---

- 1 Kamati ya Serikali za Nchi husika inayohusu kulinda na kukuza vielelezo vya tamaduni anuwai ambayo hapa inarejelewa kama “Kamati ya Serikali za Nchi husika” itaanzishwa ndani ya UNESCO. Itahusisha wawakilishi kutoka katika Nchi 18 Husika katika Makubaliano haya, na ambao wamechaguliwa na Kongamano la Nchi Husika kwa kipindi cha miaka minne wakati wa kuidhinishwa kwa Makubaliano haya kulingana na Kifungu cha 29.
- 2 Kamati ya Serikali za Nchi Husika itakutana kila mwaka.
- 3 Kamati ya Serikali za Nchi Husika itafanya kazi chini ya mamlaka na uongozi wa Kongamano la Nchi Husika pamoja na kuwajibika kwalo.
- 4 Wanachama wa Kamati ya Serikali za Nchi Husika wataongezwa hadi kufikia 25, iwapo nambari ya nchi wanachama wa Makubaliano haya itafikia watu 50.
- 5 Uchaguzi wa wanachama wa Kamati ya Serikali za Nchi Husika utazingatia kanuni za usawa wa uwakilishi wa kijioografia na kwa mzunguko wa wanaochaguliwa.
- 6 Bila mapendeleo kuhusu yale majukumu mengine ambayo Kamati ya Serikali za Nchi Husika imepewa na Makubaliano haya, shughuli za Kamati hii zitahusisha:

- a) Kuendeleza malengo ya Makubaliano haya, kuhimiza na kufuatilia utekelezaji wa malengo hayo;
  - b) Kutayarisha na kuwasilisha mipangilio ya utendakazi, kama inavyohitajiwa na Kongamano la Nchi Husika ili iweze kuidhinishwa kwa minajili ya kutekeleza na kutumiwa kulingana na masharti ya Makubaliano haya;
  - c) Kupitisha ripoti za Nchi Husika za Makubaliano haya kwa Kongamano la Nchi Husika, zikiwa na maoni na muhtasari wa yote yaliyomo;
  - d) Kutayarisha mapendekezo yanayofaa kuzingatiwa kutokana na mambo yanayoletwa mbele yake na Nchi Husika za Makubaliano haya, na kwa kuzingatia masharti husika ya Makubaliano hasa kwenye Kifungu cha 8;
  - e) Kuanzisha taratibu na njia zingine za kushauriana zinazodhamiria kuendeleza malengo na kanuni za Makubaliano haya katika mikutano mingine ya kimataifa;
  - f) Kutekeleza majukumu mengine yoyote kama yatakavyotakikana na Kongamano la Nchi Husika.
- 7) Kulingana na Sheria na Taratibu zake, Kamati ya Serikali za Nchi Husika wakati wowote inaweza kualika mashirika ya kibinafsi au ya umma, au hata watu binafsi kushiriki katika mikutano yake ili kushauriana kuhusu masuala mahususi.
- 8) Kamati ya Serikali za Nchi Husika itatayarisha na kuliwasilishia Kongamano la Nchi Husika sheria na taratibu zake za kazi ili kuidhinishwa.

## KIFUNGU 24

# OFISI YA UNESCO

---

---

---

- ① Matawi ya Makubaliano haya yatasaidiwa na Ofisi ya UNESCO.
- ② Ofisi hii itatayarisha nyaraka za Kongamano la Nchi Husika na za Kamati ya Serikali za Nchi Husika pamoja na ajenda za mikutano, na itasaidia pia katika kushughulikia ripoti zao au pia kuripoti juu ya utekelezaji wa maamuzi yao.



# IBARA ZA MWISHO

---

## KIFUNGU 25

# KUSULUHISHA MIGOGORO

---

---

---

- 1 Iwapo kuna mgogoro baina ya Nchi Husika kuhusu ufasiri au utekelezaji wa Makubaliano haya, nchi hizo zitatafuta suluhu kupitia kwa majadiliano.
- 2 Iwapo Nchi Husika haziwezi kuafikiana kupitia kwa majadiliano, zinaweza kwa pamoja kutafuta suluhu kupitia kwa ofisi za nchi nyingine au kuomba upatanisho kutoka kwa nchi nyingine.
- 3 Iwapo ofisi hizo au upatanisho haviwezi kufanyika, au iwapo hakuna suluhu yoyote iliyoafikiwa kupitia kwa majadiliano katika ofisi hizo au kupitia kwa upatanisho, Nchi Husika inaweza kutafuta msaada wa kupatanishwa kulingana na utaratibu ulioko katika Kiambatisho cha Makubaliano haya. Nchi Husika hazina budi kuzingatia kwa imani pendekezo lililofanywa na Kamisheni ya Upatanisho kuhusu kutatuliwa kwa mgogoro.
- 4 Wakati wa kuidhinisha na kukubali kutumiwa kwa Makubaliano haya, kila Nchi Husika inaweza kutangaza kwamba haitambui utaratibu wa upatanisho ulioonyeshwa hapo juu. Nchi yoyote Husika itakayokuwa imetoa tangazo kama hili, inaweza pia kuondoa tangazo hilo wakati wowote kupitia kwa taarifa kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO.



## KIFUNGU 26

# KUIDHINISHA, KUKUBALI AU KUJIUNGA NA MAKUBALIANO KWA NCHI WANACHAMA

---

---

---

- 1 Makubaliano haya hayana budi kuidhinishwa, kukubaliwa na kutumiwa na Nchi wanachama wa UNESCO kulingana pia na taratibu za katiba zao.
- 2 Uthibitisho wa kukubali kuyatumia utawasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO.

## KIFUNGU 27

# KUJIUNGA NA MAKUBALIANO

---

---

---

- 1 Makubaliano haya yatakuwa wazi kukubaliwa na nchi zote ambazo si wanachama wa UNESCO, lakini ni wanachama wa Umoja wa Mataifa au mashirika yoyote ya Umoja huu ambayo yamealikwa na Kongamano Kuu la UNESCO ili kushiriki katika kuyakubali.
- 2 Makubaliano haya pia yatakuwa wazi kukubaliwa na nchi ambazo zinafurahia mamlaka ya serikali zao za ndani ambazo zimetambuliwa na Umoja wa Mataifa lakini hazijapata uhuru kamili kulingana na azimio la 1514 (XV) la Baraza Kuu, na ambazo zina ufahamu wa maswala yaliyomo katika

Makubaliano haya pamoja na uwezo wa kuingia katika mikataba kulingana na maswala kama haya.

3 Mashirika yafuatayo yanahusu yale ya kimaeneo ya muungano wa kiuchumi:

- a) Makubaliano haya yako wazi kukubaliwa na kutumiwa na shirika lolote la kimaeneo la muungano wa kiuchumi na ambalo pia litafungwa na masharti ya Makubaliano haya sawa na nchi wanachama za Umoja wa Mataifa, isipokuwa kama inavyoelezwa hapo chini;
- b) Ikitokea kwamba nchi moja mwanachama au zaidi za shirika kama hilo pia ni Nchi Husika katika Makubaliano haya, basi shirika hili pamoja na nchi hiyo au nchi hizo wanachama zitaamua kuhusu kazi zitakazofanya katika kutekeleza majukumu ya Makubaliano haya. Ugawaji wa kazi hizo utanza kutekelezwa baada ya kukamilika kwa utaratibu wa kutoa taarifa unaoelezwa katika aya ndogo ya (c). Shirika linalohusika pamoja na nchi zake ambazo ni wanachama hazitakuwa na kibali cha kutekeleza haki zao kwa pamoja chini ya Makubaliano haya. Zaidi ya haya, mashirika ya kimaeneo ya muungano wa kiuchumi, kwa uwezo wao yanaweza kutumia haki yao ya kupiga kura kwa idadi ya kura sawa na kura za nchi zao ambazo ni wanachama, na ambazo pia ni Nchi Husika za Makubaliano haya. Shirika kama hilo pia haliwezi kutumia haki yake ya kupiga kura iwapo nchi yake ambayo pia ni mwanachama itatumia haki hiyo au pia kinyume chake;
- c) Shirika la kimaeneo la muungano wa kiuchumi na nchi yake au nchi zake wanachama ambazo zimekubali kugawanya kazi kama inavyoelezwa katika ibara ya (b), litazijulisha Nchi Husika kuhusu mgao wowote wa kazi

kwa njia ifuatayo:

- i) Katika uthibitisho wake wa kuyakubali Makubaliano haya, shirika hilo litatangaza wazi mgao wa kazi zake kulingana na yale yanayozingatiwa katika Makubaliano hayo;
  - ii) Iwapo kutatokea mabadiliko ya kazi hizo baadaye, shirika la kimaeneo la muungano wa kiuchumi litamfahamisha mweka amana kuhusu mapendekezo ya mabadiliko ya kazi hizo, naye mweka amana atazijulisha Nchi Husika juu ya mabadiliko hayo.
- d) Nchi wanachama ambazo ni za shirika la kimaeneo la muungano wa kiuchumi zinakuwa Nchi Husika za Makubaliano haya na zitachukuliwa kuwa zenye uwezo wa maswala yote ya kujua ni uhamisho upi wa ujuzi wa shirika hilo ambao haujatangazwa au kujulishwa kwa mweka amana;
- e) “Shirika la Kimaeneo la Muungano wa Kiuchumi” humaanisha shirika linalojumuisha mataifa huru, ambayo pia ni wanachama wa Umoja wa Mataifa, au shirika lolote maalumu chini ya Umoja huu ambalo mataifa hayo yamehamisha uwezo wao unaohusisha maswala ya Makubaliano haya, na ambalo limeruhusiwa kuwa mhusika katika Mkubaliano hayo kulingana na taratibu zake;
- 4 Uthibitisho wa kukubali na kujiunga na Makubaliano haya utawasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO.

## KIFUNGU 28

### PAHALI PA KUWASILIANA

---

---

---

Baada ya kuwa Nchi Husika za Makubaliano haya, kila Nchi Husika itachagua pahali maalumu pa kuwasiliana kama inavyorejelewa katika Kifungu cha 9.

## KIFUNGU 29

### KUANZA KUTUMIKA

---

---

---

- ① Makubaliano haya yataanza kutumika miezi mitatu baada ya tarehe ya kuwasilisha uthibitisho wa thelathini wa kukubali kuyatumia Makubaliano lakini hapa ni kwa zile nchi au mashirika ya kimaeneo ya muungano wa kiuchumi ambayo yamewasilisha uthibitisho wao wa kukubali kuyatumia Makubaliano haya kwenye tarehe hiyo ya kuwasilisha au kabla. Makubaliano yataanza kutumiwa na Nchi Husika nyingine yoyote miezi mitatu baada ya kuwasilisha uthibitisho wa kukubali kuyatumia.
- ② Kwa mujibu wa Kifungu hiki, uthibitisho wowote utakaowasilishwa na shirika la kimaeneo la muungano wa kiuchumi hautachukuliwa kama nyongeza za uthibitisho unaowasilishwa na nchi wanachama wa shirika hilo.

## KIFUNGU 30

# MIFUMO YA KIKATIBA YA KIMAJIMBO

---

---

---

Kwa kutambua kwamba Nchi Husika hazina budi kutii maafikiano ya kimataifa bila kujali mifumo yao ya kikatiba, masharti yafuatayo yanahusu hizo Nchi Husika zilizo na mifumo ya kikatiba ya kimajimbo au isiyo na mfumo mmoja wa kiutawala:

- a) Kulingana na masharti ya Makubaliano haya ambayo utekelezaji wake uko chini ya mamlaka ya kisheria ya serikali ya majimbo au yenye mamlaka makuu ya kisheria, majukumu ya serikali hizo mbili yatakuwa sawa kama ya zile Nchi Husika ambazo si za kimajimbo;
- b) Kulingana na masharti ya Makubaliano haya ambayo utekelezaji wake uko chini ya mamlaka ya utawala mahususi kama vile wa nchi, kaunti au mikoa na ambayo haishurutishwi na mfumo wa kikatiba wa kimajimbo kuchukua hatua za kisheria inapohitajika, serikali ya majimbo itafahamisha mamlaka za serikali mahususi kama vile za nchi, kaunti au za mikoa kuhusu masharti ya Makubaliano pamoja na mapendekezo ya jinsi ya kuyakubali.

## KIFUNGU 31

# KUFUTA MAKUBALIANO

---

---

---

- ① Nchi husika yoyote katika Makubaliano haya inaweza kuyafutilia mbali.
- ② Kufuta Makubaliano kutafanywa kwa njia ya uthibitisho wa kimaandishi utakaowasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO.
- ③ Kufuta Makubaliano kutaanza kutumika miezi 12 baada ya uthibitisho huo kupokewa. Hili halitaathiri majukumu ya kifedha ya Nchi Husika inayofuta Makubaliano hayo mpaka pale tarehe ya kujiondoa kwa Nchi hiyo Husika itakapofika.

## KIFUNGU 32

# SHUGHULI ZA UHIFADHI

---

---

---

Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO ambaye ndiye mhifadhi wa Makubaliano haya atazifahamisha nchi wanachama za Umoja wa Mataifa, nchi zisizo wanachama pamoja na mashirika ya kimaeneo ya muungano wa kiuchumi yanayorejelewa katika Kifungu cha 27 pamoja na Umoja wa Mataifa kuhusu mawasilisho ya uthibitisho wa kukubali kujiunga na Makubaliano haya kama inavyoelezwa katika Vifungu vya 26 na 27, na ufutaji wa Makubaliano kama inavyoelezwa katika Kifungu cha 31.

## KIFUNGU 33

# MASAHIHISHO

---

---

---

- 1 Nchi Husika ya Makubaliano haya inaweza kupendekeza masahihisho katika Makubaliano haya kwa kuwasiliana na Mkurugenzi Mkuu kimaandishi. Mkurugenzi huyo atasambaza mawasilisho hayo kwa Nchi Husika zote. Iwapo kufikia miezi sita tangu kusambazwa kwa mawasiliano hayo, idadi chini ya nusu ya Nchi Husika haikutoa majibu ya kuridhisha kutokana na ombi hilo, Mkurugenzi Mkuu atawasilisha pendekezo hilo katika kikao kinachofuata cha Kongamano la Nchi Husika ili kujadiliwa na kukubaliwa.
- 2 Masahihisho yatakubaliwa na thuluthi mbili ya Nchi Husika zinazohudhuria na kupiga kura.
- 3 Yanapokubaliwa, masahihisho ya Makubaliano hayo yatawasilishwa kwa Nchi Husika ili kuidhinishwa na kukubaliwa kutumika.
- 4 Kwa Nchi Husika zilizoidhinisha na kukubali yatumike, masahihisho hayo yataanza kutumika miezi mitatu baada ya kuwasilishwa kwa uthibitisho unaorejelewa kwenye ibara ya 3 ya Kifungu hiki na thuluthi mbili ya Nchi Husika. Baada ya hapo, kila Nchi Husika inayoidhinisha na kukubali masahihisho hayo kutumika, haya yataanza kutumika miezi mitatu baada ya tarehe ambapo Nchi Husika iliyopendekeza masahihisho hayo ilipoyawasilisha ili yaidhinishwe na kukubaliwa kutumika.
- 5 Utaratibu uliowekwa kwenye ibara za 3 na 4 hautahusisha

masahihisho ya Kifungu cha 23 kuhusu idadi ya wanachama wa Kamati ya Serikali za Nchi. Masahihisho kama hayo yataanza kutumika wakati yanapokubaliwa.

6 Nchi au shirika la kimaeneo la muungano wa kiuchumi linalorejelewa katika Kifungu cha 27 na ambalo linakuwa nchi au shirika husika la Makubaliano haya baada ya masahihisho kukubaliwa kutumika kulingana na ibara ya 4 ya Kifungu hiki bila kutoa maoni yao, nchi au shirika hilo litachukuliwa kuwa:

- a) Nchi au shirika husika la Makubaliano yaliyosahihishwa; na
- b) Nchi au shirika husika la Makubaliano hayo yasiyosahihishwa kuhusiana na nchi au shirika lolote husika lisilofungamanishwa na masahihisho hayo.

## KIFUNGU 34

### MATINI ZENYE MAMLAKA

---

---

---

Makubaliano haya yako katika lugha za Kiarabu, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kirusi na Kihispania, na matini zote sita zina mamlaka sawa.



## KIFUNGU 35

### USAJILI

---

---

---

Kulingana na Kifungu cha 102 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Makubaliano haya yatasajiliwa katika ofisi ya Umoja wa Mataifa kupitia kwa ombi la Mkurugenzi wa UNESCO.



# TARATIBU ZA UPATANISHO

## KIFUNGU 1 KAMISHENI YA UPATANISHO

---

---

---

Kamisheni ya Upatanisho itaundwa kupitia kwa ombi la mojawapo ya Nchi Husika katika mgogoro. Isipokuwa pale ambapo Nchi hizo Husika zimekubaliana, Kamisheni hiyo itakuwa na wanachama watano, wawili wakiwa wamechaguliwa na kila Nchi inayohusika katika mgogoro huku Rais akichaguliwa na wanachama hao.

## KIFUNGU 2 WANACHAMA WA KAMISHENI

---

---

---

Ikiwa kuna mgogoro unaohusisha zaidi ya Nchi mbili Husika, zile nchi ambazo ziko upande mmoja zitachagua wanachama wao wa Kamisheni kwa kukubaliana pamoja. Pale ambapo Nchi Husika mbili au zaidi zina mapendeleo tofauti au kuna

kutoelewana kuhusu iwapo zote zinapendelea upande mmoja, basi kila Nchi Husika itachagua mwanachama wake tofauti na wengine.

## KIFUNGU 3

### UTEUZI

---

---

---

Ikiwa hakuna uteuzi wowote uliofanywa na Nchi Husika katika muda wa miezi miwili tangu kutolewa kwa ombi la kuunda Kamisheni ya Upatanisho, Mkurugenzi Mkuu atafanya uteuzi huo wa wanachama ndani ya muda wa miezi miwili zaidi, na iwapo ataulizwa kufanya hivyo na Nchi Husika iliyotuma ombi hilo.

## KIFUNGU 4

# RAIS WA KAMISHENI

---

---

---

Ikiwa Rais wa Kamisheni ya Upatanisho hajachaguliwa katika muda wa miezi miwili baada ya kuteuliwa kwa mwanachama wa mwisho wa wanachama wa Kamisheni, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO atamteua Rais kushikilia cheo hicho ndani ya muda wa miezi miwili zaidi, iwapo ataulizwa kufanya hivyo na mojawapo ya Nchi Husika.

## KIFUNGU 5

# MAAMUZI

---

---

---

Kamisheni ya Upatanisho itafanya maamuzi yake kupitia kwa wingi wa kura za wanachama wake. Pia itaamua utaratibu wake wa maamuzi isipokuwa pale ambapo Nchi Husika katika mgogoro zimekubaliana kuhusu utaratibu wa kufuatwa. Kamisheni itatoa pendekezo la kutatua mgogoro ambalo Nchi Husika zitazingatia kwa imani.

## KIFUNGU 6

# KUTOKUBALIANA

---

---

---

Kutokubaliana iwapo Kamisheni ya Upatanisho ina uwezo wa kufanya kazi kutaamuliwa na Kamisheni yenyewe.



Makubaliano ya 2005 ya Ulinzi na Ukuzaji wa Vielelezo vya Tamaduni Anuwai ni Mkataba wa kimataifa ambao unatoa mfumo wa sera ili kudhibiti utamaduni.

Makubaliano haya yanatambua upekee wa utamaduni kama ulio na mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na ambao unahakikisha kwamba wasanii, wataalamu wa ubunifu, weledi wa utamaduni na raia kote ulimwenguni wanaweza kubuni, kuzalisha, kusambaza na kufurahia bidhaa za ubunifu mbalimbali, huduma na shughuli za kitamaduni, zikiwemo zao wenyewe.

**Sehemu ya Vielelezo vya Tamaduni Anuwai  
Kitengo cha Ubunifu  
Sekta ya Utamaduni  
UNESCO**

7, Place de Fonteney – 75352 Paris 07, SP, France

Barua pepe: [convention2005@unesco.org](mailto:convention2005@unesco.org)

[en.unesco.org/creativity/](http://en.unesco.org/creativity/)

Tufuate kwenye Twitter: #supportcreativity